**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA CHUO CHA UTAWALA WA UMMA NAM. 1 YA 2007 NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye wingi wa Rehma, ambae ameumba Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake na kuviwekea taratibu ili zifuatwe. Pia, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha leo hii kutekeleza majukumu yetu kwa amani na usalama wa Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya maoni ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika kuuchangia na kuuboresha Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma Nam. 1 ya 2007 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akuzidishie afya njema itakayokuwezesha kutekeleza majukumu yako kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora; Mheshimiwa Mwl. Haroun Ali Suleiman kwa mashirikiano

yake makubwa aliyotupatia Kamati hii wakati wa kuupitia Mswada huu lakini pia, nje ya Mswada huu amekuwa akitupa mashirkiano makubwa sana katika kutekeleza majukumu yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu ili aweze kutusaidia zaidi katika kujenga mustakbali bora wa Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, napenda kuwashukuru watendaji wake wote katika Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wao Ndg. Mansura M. Kassim kwa kusimamia vyema na kurekebisha Sheria hii ambayo inakwenda kufanya marekebisho sambamba na Muundo Mpya wa Chuo Cha Utawala wa Umma ulioidhinishwa na Serikali mwaka jana.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa niwashukuru wadau wote wa Mswada huu ambao wameupitia kwa nafasi zao lakini pia wadau ambao walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao ya kujenga na kuiwezesha Kamati kupata upeo mpana zaidi katika Masuala ya Utumishi na Miundo yake katika kukuza sekta ya elimu Nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, pongezi za pekee ziende kwa wataalamu wetu wa Sheria kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa jitihada zao kubwa walizozionyesha katika kuwapatia wajumbe wa Kamati hii maarifa kuhusu mswada huu na kuwaelekeza mambo mbali mbali ambayo msingi wake ni kuufanya Mswada huu uwe bora zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, pia, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa waliyotoa kwangu na juhudi zao wakati wa kuujadili kwa kina Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha za Alama |

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa madhumuni ya Mswada huu pamoja na mambo mengine ni kufanya marekebisho ambayo yanakwenda sambamba na Muundo Mpya wa Chuo Cha Utawala wa Umma (IPA) ulioidhinishwa na Serikali mwaka uliopita ili

kukidhi mahitaji ya mfumo wa elimu ya juu pamoja na matakwa ya Baraza la Elimu ya Ufundi na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mantiki hiyo, Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeupitia Mswada huu kifungu kwa kifungu na kujiridhisha kwamba umekuwa Mswada bora na uliokidhi malengo kwa wakati mahususi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri katika jina refu la Mswada kurekebishwa na kuongezwa neno **"Mwaka"** baina ya neno **"ya"** na **"2007"** ili kwenda sambamba na uandishi wa miswada mengine tunayaoipitisha.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuweka mtiririko bora na wenye muundo unaolingana na sheria nyengine za Taasisi za elimu, Kamati yangu inashauri Kifungu cha 5(1) cha Mswada huu kurekebishwa kama ifuatavyo:

*Mosi:* Katika aya ya (b), kufutwa maneno "**anayeingia kwa nafasi yake".**

*Pili:* Katika aya ya (c), kufutwa neno **"Msaidizi"** na kuwekwa badala yake neno **"Naibu".**

*Tatu:* Katika aya ya (d), kufutwa neno **"Msaidizi"** na kuwekwa badala yake neno **"Naibu".**

**Mheshimiwa Spika,** aidha, katika kukipa nguvu na uwezo wa kusimamia malengo ya Chuo na kuwafanya watendaji wawe na

uhuru wa utekelezaji wa majukumu yao, Kamati inapendekeza kuongeza maneno katika Kifungu cha 8 kwa kurekebishwa katika kifungu kipya cha 10(4)(b), kwa kuongezwa maneno **"pamoja na miongozo inayotolewa na Chuo"** Mwishoni mwa aya hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, inashauri Kifungu cha 9 kurekebishwa katika kifungu kipya cha 11(2), kwa kufutwa na badala yake kuandikwa upya kama ifuatavyo:

> **"Baraza litateua Wakuu wa idara za Chuo kutokana na mapendekezo ya Mkuu wa Chuo kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma"**.

**Mheshimiwa Spika,** katika Kifungu cha 11 cha Mswada huu Kamati inashuri kurekebishwa katika kifungu kipya cha 14(2), kwa kufuta neno **"mujibu"** liliopo baina ya neno **"kwa"** na **"wa"** na kuwekwa badala yake neno "**kuzingatia**" ili kwenda sambamba na muktadha uliokusudiwa katika kifungu hiki.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na mapendekezo hayo, Kamati yangu imeenda mbali zaidi katika Mswada huu kwa kuipitia upya Sheria Mama na kugundua kasoro moja ambayo haikuzingatiwa katika Mswada huu. Kwa mnasaba huo, Kamati inashauri kuongezwa kifungu kipya cha 12 kitakachorekebisha kifungu cha 16 cha Sheria Mama kwa kufutwa maneno **"kuanzishwa kwa sheria ya Mdhibiti Mkuu Nam. 11 ya Mwaka 2003"** na kuweka badala yake maneno **"kuanzishwa kwa**

**Sheria ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali"** kwani hii ndio sheria sahihi iliyopo na inayotumika.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hotuba hii kwa kuwashauri wajumbe wa Baraza lako Tukufu wakubaliane na maoni ya Kamati yetu katika Mswada huu kwani Kamati imepata mafunzo ya kutosha juu ya Mswada huu ili kuufanya uwe bora na wenye kuleta maslahi kwa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati yetu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu waujadili na kuuchangia ipasavyo Mswada huu na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itaenda kuwa chachu ya maendeleo katika sekta ya elimu hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** **Naomba Kuwasilisha**.

Ahsante,

..............................

**(*Machano Othman Said*)**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**